

transforming age®

# Utamaduni wa Ubora©

Kuunganisha dhamira na maadili yetu

**Kubadilisha mtazamo kuhusu umri ni msingi wa kila kitu tunachofanya.**

# Tunageuza Umri.

Dhamira yetu ni kuunda mazingira ya suluhisho fanisi za uzee na maisha marefu kote katika mpangilio wa uchumi wa kijamii ambazo humweka mzee mkongwe kwanza. Falsafa yetu ya Mteja Mmoja inalenga kuwezesha kuzeeka kwa mafanikio na kuendeleza maisha marefu yenye afya. Tunajenga dhamira yetu kupitia kwa nguzo zetu tano za dhamira za makazi, huduma za jamii, ushirika, teknolojia, na uhisani.  Suluhisho zetu zilizounganishwa na zinazozingatia kumlenga mtu binafsi huwafikia watu walipo na kuwasaidia katika maisha yote.

Nembo yetu inawakilisha dhamira hii, kwa kuleta nguzo zetu tano pamoja kumzunguka huyo Mteja Mmoja katika kila kitu tunachofanya.

## Maono yetu ni kuwezesha kuzeeka kwa ufanisi na kuendeleza maisha marefu yenye afya.

Tunaamini kwamba wazee wakongwe huimarisha jamii, na kote kwenye mtandao wetu wa washirika tunashughulika kupanua kile kinawezekana huku maisha yakizidi kuwa marefu. Huwa tunatetea heshima, miunganisho, na lengo ili maisha marefu yawe maisha bora. Kupitia kwa huduma zetu, jamii, na ushirika, tunaweza kuunda mazingira ambako wazee wakongwe wanaweza kufanikiwa wakiwa na uzima kamili wa mtu, umiliki, na furaha.

"Kwa pamoja, kama mtandao mmoja unaohudumia mteja mmoja kwa wakati mmoja, **tunasaidia watu kuwa na miaka yenye maana**, sio tu miaka mingi."

"**Kubadilisha mtazamo kuhusu** umri ni shughuli yetu ya kila siku na ahadi yetu ya muda mrefu."

"Kuzeeka sio tatizo la kusuluhisha. **Ni mageuzi ya kujitwalia.**"

**– Torsten Hirche**
Rais na Mkurugenzi Mkuu

# Nguzo Zetu 5 za Dhamira

## Makazi

Tunapeana makazi ambayo yanaunga mkono usalama, starehe, kusudi, na uunganishaji—kuunda jamii ambapo wazee wakongwe wanaweza kuzeeka katika mahali palipotengeka na penye umiliki.

## Huduma za Kijamii

Tunawasaidia wazee wakongwe kukaa wakijitegemea na wenye shughuli kwa kuwatimizia mahitaji yao ya kila siku na kuimarisha mahusiano ya kijamii kwa ajili ya afya bora na ustahimilivu.

## Uhisani

Tunapanua ufikiaji na kupunguza ukosefu wa usawa kwa kufadhili mafunzo bora ya walezi, ujuzi bora kwa wakazi, na jamii stahimilivu zaidi na nafuu.

"**Tunachagua kuwa nguvu chanya** kazini na katika timu yetu, kusaidiana, na kufanya kazi yetu bora kila siku na kwa kila mwingiliano."

## Ushirikiano

Tunashirikiana na washirika wanaounga mkono dhamira ili kupanua nyenzo, kuboresha huduma, na kuleta uvumbuzi unaoboresha ubora wa maisha kwa wazee wakongwe.

## Teknolojia

Huwa tunafanya utunzaji kuwa wa kibinafsi zaidi, unaofikika, na ufanisi kupitia teknolojia ambayo inasaidia usalama, uhuru, na utoaji bora wa malezi.



# Utamaduni wa Ubora

**Utamaduni** ni mkusanyiko wa imani za pamoja, maadili, kanuni, na tabia ambazo zinaonyesha na kusaidia kufafanua kikundi cha watu.

**Ubora** una maanisha kujisatiti kuwa bora zaidi. Pia inamaanisha kuboresha na kujifunza kadri muda unavyosonga na matokeo bora.







"Tunapounda **uwezo usio na kikomo** kwa wateja wetu na wakazi, kila mmoja wetu anaunda uwezekano usio na kikomo wa kushawishi timu yetu."

# COE-nnecting the Dots

**Utamaduni wa Ubora (COE)** huunganisha maudhui ya dhamira, maadili na malengo yetu.

**Kila mmoja wetu** anachangia dhamira yetu na malengo yetu kwa kutoa ubora na kuonyesha maadili yetu.







# Maadili yetu

**Kuunda uzoefu mwema** kwa washiriki wa timu yetu au kwa wakazi/wateja wetu, tuna nafasi ya kuishi kulingana na maadili yetu. Jinsi tunavyowasalimu watu, jinsi tunavyowajali na kuinua watu, jinsi tunavyofanya mambo yaliyo sahihi — kila siku.

## Uadilifu

- Tunatenda kwa uaminifu, na tunafanya mambo yaliyo sahihi.
- Tunatenda kwa kujitolea, na ukweli.
- Tunafanya kazi kwa bidii ili kupata uaminifu na kuonyesha kuwa tunaaminika.

## Ushirikiano

- Tunafanya kazi pamoja na tunasaidiana.
- Tunathamini mchango wa kila memba wa timu.
- Tunaongoza kwa mfano katika kuwatumikia wakazi wetu na wateja.

## Heshima

- Tunaheshimu na kukubali thamani ya kila mtu.
- Tunatambua na kuthamini utofauti wa timu yetu, wakazi wetu na wateja wetu.

## Neema

- Tunaonyesha fadhili, huruma, na upendo kwa wote.
- Tunasherehekea na tunakubali tofauti katika kila mmoja.
- Tunajali timu yetu na tunaowahudumia.

## Raha

- Tunafurahi.
- Tunaleta furaha kwa kazi yetu, timu yetu, wakazi wetu, na wateja wetu.
- Tunajua mtazamo mzuri unachangia ubora.

## Uvumbuzi

- Tunatambua fursa za kuwa bora kila siku.
- Tunashiriki maoni ya kuboresha jinsi tunavyofanya kazi.
- Tunafanya kazi pamoja kuunda suluhisho mpya.

## Kuwajibika

- Tunawajibika kwa vitendo vyetu.
- Tunamjulisha msimamizi wetu ikiwa tumefanya kosa, ili liweze kurekebishwa haraka.
- Tunadumisha viwango vya ubora wa juu.

# Malengo Yetu ya Kimkakati

Kila siku, kazi tunayofanya sote ni muhimu katika kuendeleza dhamira yetu na malengo ya kimkakati.


- **Kuwa kiongozi katika uzeekaji wa ufanisi na maisha marefu** kwa kuishi Utamaduni wa Ubora wa kila siku.
- **Kua na uwe Mbunifu** huku tunapowekeza upya katika programu na mipango ili kupanua kazi zetu.
- **Kuwa wa kipekee. Kuunda suluhisho na huduma** ambazo hufurahisha watu, uboresha ujuzi, na uwezesha safari ya kuzeeka yenye ufanisi—huku zikibaki nafuu na zinazofikikiwa.
- **Kuwa yule mwajiri anayependelewa na kuongoza kwa mfano** kupitia kwa Tamaduni yetu ya Ubora, kuweka viwango vya juu kwa ajili ya watu, bidhaa, na michakato.
- **Kuwa shirika linaloendelezwa na data na maarifa** kwa kutumia matokeo na maoni ili kufanya maamuzi haraka na kwa ufanisi.
- **Kupanua kipimo chetu cha utendaji.** Watu, Faida na Sayari. Huwa tunakabili matatizo magumu ana kwa ana kwa ufanisi wa kiutendaji na kimazingira endelevu, kuwekeza upya na kupanua utendaji wetu.



# Wazo bora hushinda, si cheo kwenye shirika.

## Timu Moja

Muda wetu, juhudi, bidii, na mtazamo hujenga Utamaduni wa Ubora. Kila siku, huwa unachangia harakati inayoboresha maisha, ikiongozwa na imani yetu katika uongozi wa utumishi na kujitolea kwetu kutumikia kwa kusudi na unyenyekevu.



# Tamaduni ya Ubora Ikifanya Kazi

Ubora sio kile tu tunakazania. Ni kile tulicho. Kila siku, tunafungulia uhai wa dhamira yetu kwa kuhudumiana kwa moyo mkunjufu, kuongoza kwa uadilifu, na kuunda jamii na majukwaa salama yanayostawi. Kwa pamoja, tumeweka viwango vya juu zaidi na tunazifikia kwa roho chanya, ya ninaweza kufanya. Vitendo hivi vinatudhihirisha na kutupatia hamasa ili tuwatendee kwa ubora zaidi wakazi, wateja, na kila mmoja.

## Huduma Bora

### Tunafanya Mfano ulio Bora Zaidi:

- **Tunamtendea kila mtu** kwa wema, huruma na heshima—kila wakati.
- **Tupo kikamilifu:** huwa tunawasalimu walio karibu nasi na kupeana umakinifu wetu kwa mtu aliye mbele yetu.
- **Huwa tunawasiliana** kwa kitaalamu na furaha katika kila utangamano.
- **Huwa tunafuata** viwango vya usafi na mavazi ili kuonyesha ufanisi.
- **Huwa tunapunguza** vifaa vya kielektroniki vya kibinafsi kwa mapumziko na kupunguza matumizi ya simu tukiwa na wengine.
- **Huwa tunadumisha** mazungumzo yakiwa ya kitaalamu na kwa sauti inayofaa.

## Huwa tunafanya kazi tukiwa na Fikra ya Mmiliki:

- **Huwa tunawajibikia** matokeo mazuri na huwa tunafanya maamuzi yaliyowezeshwa.
- **Huwa tunaonyesha** maadili yetu kwa shauku na kusudi katika yote tufanyayo.
- **Huwa tunajitolea kwa mafanikio** ya dhamira yetu, timu yetu, na wale tunaohudumia.

"Nimejifunza kuwa watu watasahau kile ulichosema, watu watasahau kile ulichofanya, lakini watu hawatasahau **jinsi ulivyowafanya wahisi.**"

- Maya Angelou



## Huwa Tunatoa Ujuzi Madhubuti:

- **Tunatoa suluhisho** kwa maswali au wasiwasi—kamwe usimuache mtu bila jibu.
- **Huwa tunauliza,** “Je, Kuna kitu kingine chochote ninaweza kukufanyia?” kabla ya kumaliza kila mazungumzo.
- **Huwa tunawasindikiza wateja na wakazi** wakati tunapowapa mwelekeo au kutafuta mtu ambaye anaweza.
- **Huwa tunakubali maswali au wasiwasi** kwa kutumia H.E.A.R. (Hear, Empathize, Apologize, Resolve).

H **Sikiza suala.** Tunasikiliza kwa makini ili kuhakikisha tunaelewa.

E **Hurumia.** Tunaonyesha tunaelewa maoni yao na jinsi wanavyohisi.

"**Kwa sababu ya tabasamu lako**, unafanya maisha kuwa mazuri zaidi.”

- Thich Nhat Hahn

A **Omba msamaha.** Kwa suala na kwa usumbufu wowote ambao hili linaweza kuwa limewasababishia.

R **Suluhisha.** Fanya kadri ya uwezo wako kusuluhisha tatizo au kutafuta mtu anayeweza kulisuluhisha.

# Uongozi Bora

## Tunaongoza kwa Mfano:

- **Sisi sote ni viongozi.** Huwa tunafanya mambo yaliyo sahihi na kuhudumiana mmoja kwa mwingine.
- **Sisi ni wadadisi na mahiri.**
- **Tunaheshimu tofauti za kitamaduni** na kukumbatia utofauti, usawa, na uhusishaji.
- **Huwa tunawasaidia wanatimu** na kuwachukulia kuwa wenye nia njema.
- **Huwa tunazungumza** tunapoona fursa za uboreshaji.
- **Tunachangia** kwa mazingira chanya ya kazi na mazuri—haswa wakati wa mfadhaiko.
- **Tunajiwajibisha wenyewe** na wengine.
- **Huwa tunahakikisha** wazo bora ndilo hushinda—si cheo.
- **Wakati uamuzi unapofanywa**, huwa tunajitolea kwake na kusonga mbele.
- **Huwa tunatatua migogoro haraka** na kwa kiutaalamu.
- **Huwa tunakaribisha** wanatimu wapya kwa furaha na uhusishaji.

## Huwa Tunapata Matokeo:

- **Huwa tunakubali uwajibikaji** kwa matendo na matokeo yake.
- **Huwa tunafanya kadri ya uwezo wetu** na tunao mtazamo wa ninaweza kufanya.
- **Huwa tunafanya kazi zetu kwa usahihi na vizuri,** na tunafanya kikamilifu majukumu kulingana na maelezo ya kazi yetu.

- **Tunatoa** matokeo ya ubora wa juu kwa ajikli ya mafanikio makubwa.
- **Huwa tunasonga kwa malengo** na kuchukua hatua bila kuahirisha mambo.
- **Huwa tunatarajia mahitaji** na kufikiria matokeo maradufu yasiyotarajiwa.
- **Tuna mazoea ya kutumia kwa uangalifu** na kupunguza gharama. Hatuharibu vitu.
- **Tunang'ang'ana ili kujikimu kifedha—**pasipo faida ya kifedha hakuna dhamira. Kila mhusika lazima awe imara kifedha ili kugharamia dhamira.
- **Huwa tunaendelea** kuimarisha ujuzi na kusonga mbele kila siku.
- **Huwa tunasimamia** mikutano kwa ufanisi ili kuzidisha muda wa kuwahudumia wakazi na wateja.
- **Huwa tunadumisha mambo yakiwa** rahisi na kuzingatia malengo.

## Huwa Tunatoa Mawasiliano Mazuri:

- **Huwa tunatambua** kazi zilizofanywa vizuri na kutoa shukrani.
- **Sisi ni wenye Uwazi** na tunakaribisha majadiliano wazi—hata wakati hatukubaliani.
- **Huwa tunashughulikia kutokubaliana** moja kwa moja pamoja na wale wanaohusika.
- **Tunaheshimu usiri** na kutumia uamuzi wakati tunapochukua au kushiriki taarifa.
- **Hatufanyi umbea**—kamwe.

- **Huwa tunazungumza kwa sauti ya kitaalamu** na huwa tunainua sauti zetu tu kwa ajili ya usalama.
- **Huwa tunawasiliana kwa ufupi** tukitumia W5 na H1 (Kwanini, Nini, Nani, Lini, Wapi, Vipi).
- **Huwa tunajibu jumbe** (baruapepe, arafa, barua ya sauti) ndani ya saa 24, wakati wowote inapowezekana.

## Usalama Madhubuti na Uzingatiaji

### Tunakuza Usalama Madhubuti:

- **Huwa tunaripoti na kushughulikia** hali au vitendo visivyo salama mara moja ili kumlinda kila mmoja.
- **Huwa tunafuatilia habari za kisasa** kuhusu kifaa cha usalama na kusaidia wakazi na wateja katika matumizi yake yanayofaa.
- **Huwa tunawakumbusha** wengine kuhusu taratibu za usalama na kushiriki kikamilifu katika mazoezi na mafunzo.
- **Huwa tunafuata maelekezo yote** kwa mifumo ya kompyuta za kazi, na vifaa ili kudumisha usalama pamoja na mazoezi ya usalama na mafunzo.

### Tunaunda Mazingira Salama kwa Kila Mmoja:

- **Tunakaa chonjo tukijua** mazingira yetu nyakati zote.
- **Tunadumisha** maeneo ya kazi yakiwa nadhifu, safi, na ya kitaalamu.
- **Huwa tunazoa** na kutupa takataka bila kuchelewa.
- **Tunaripoti** fanicha zilizovunjika, vifaa au vyombo bila kuchelewa.

## Tunahakikisha Uzingatiaji:

- **Tunalinda** usiri—kamwe hatupeani taarifa ya mkazi, mteja, biashara, au mwanatimu bila idhini.
- **Tunajua** na kufuata matakwa ya uzingatiaji na kisheria ya majukumu yetu.
- **Tunaripoti** vitendo vyovyote vinavyoshukiwa au vinavyojulikana kuwa vya vurugu, unyanyasaji wa wazee au kutelekezwa, unyanyasaji, uonevu, wizi, au udanganyifu haraka.
- **Tunaripoti** shughuli zinazoshukiwa au vitu bila kuchelewa.
- **Tunatumia** Simu ya Dharura (1-800-275-9575), transformingage.org, au msimbo wa QR kwa wasiwasi ambao unatushinda kuripoti kwa usimamizi.



"Watu hawajali ni kiasi gani unajua hadi wajue ni**kiasi gani unavyojali."**"

- Theodore Roosevelt



# COE-nnecting the Dots

Kwa kuwa kila mmoja ana kazi yake kwenye dhamira yetu ya kuwahudumia wazee wakongwe, tunakuhimiza ufikirie kuhusu maswali haya na uhusianishe dhamira, maadili na malengo.

- **Je, Utamaduni unamaanisha nini kwako?**
- **Ubora unamaanisha nini kwako?**
- **Je, Unajiunganishaje na dhamira yetu na maadili yetu?**
- **Ni nukuu gani zinazokuhimiza kufanya kadri ya uwezo wako?**

Dhamira — Maadili — Malengo



# ASANTE

Asante kwa kujiunga na Familia ya Kubadilisha Umri, kuunga mkono dhamira yetu na kuboresha maisha ya wazee wakongwe. Ningependa kusikia kutoka kwako Ninakaribisha maoni yako, makubwa au madogo, kuukosoa au maoni, nitumie tu kwa baruapepe kwa ideas@transformingage.org

**Pamoja tunaweza kubadilisha ulimwengu!**



**Torsten Hirche**

Rais na Afisa Mkuu Mtendaji

TransformingAge.org
425-559-6301
© 2026 Transforming Age
Toleo la 6.0 2026